# WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI



JARIDA MAALUM

# RUVUMA

TOLEO LA NANE (8)

## YALIYOMO


01 Urasimishaji Makazi

02 Utatuzi Migogoro

03 Malengo mapya



BODI YA UHARIRI

**MARY MAKONDO**
Katibu Mkuu

**LUSAJO MWAKABUKU**
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

**WAANDISHI**
Munir Shemweta
Eliafile Solla
Hassan Mabuye
Magreth Lyimo



Mji wa Serikali Mtumba, S. L. P. 2908 | 40477- DODOMA | Simu: +255 262 963309/13/14 | Nukushi: +255 262 963316
Barua pepe: ps@lands.go.tz | Tovuti: www.lands.go.tz



*Mgeni Rasmi Mh. Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Brigadier Generally Wilbert Ibuge akifungua kikao cha wataalam wa Sekta ya Ardhi Mkoa wa Ruvuma*

# RUVUMA YAVUKA MALENGO YA URASIMISHAJI MAKAZI

- *Yarasimisha makazi kwa 114%*

**Na Lusajo Mwakabuku ,** WANMM

Moja ya malengo ambayo Mkoa wa Ruvuma ulipangiwa kwa upande wa urasimishaji kwa mwaka kuanzia tarehe 1 Julai, 2020 mpaka tarehe 30 June, 2021 ilikuwa ni kurasimisha viwanja 7500. Taarifa ya tahmini ya utendaji wa kazi iliyotolewa katika kikao cha watumishi wa sekta ya ardhi ya Mkoa wa Ruvuma imeonesha kuwa mkoa ulifanikiwa kurasimisha viwanja 8,587 na hivyo kuvuka lengo kwa asilimia 114.

Taarifa hiyo iliyotolewa na Kamishna wa Ardhi Msaidizi mkoa wa Ruvuma Ildefonce Ndemela pia ilibainisha jumla ya michoro 19 ilikamilika kwa kipndi hicho na kwamba mkoa unatajaria kurasimisha viwanja 6000 kwa mwaka ujao wa fedha.

Pamoja na mafanikio hayo yaliyopatikana, kulikuwa na changamoto mbalimbali ambazo zilipelekea kupungua kwa kasi ya urasimishaji mkoani humo, moja ya changamoto hizo ni Baadhi ya wananchi kukataa au kuchukua muda mrefu kuachia maeneo kwa ajili ya miundombinu ya barabara na huduma za jamii. Pamoja na juhudi mbalimbali za kutoa elimu na kueleza umuhimu bado kuna baadhi ya watu walifikiri wanahitaji fidia kubwa kwa huduma za kijamii hivyo vikao vilichukua muda mrefu kufikia muafaka

Changamoto nyingine ilikuwa ni kutobainishwa na kufutwa kwa upimaji ardhi hai wa zamani ambao hauendani na Maendelezo halisi katika baadhi ya maeneo ya urasimishaji kabla ya kuanza kwa zoezi la urasimishaji na hivyo kuchelewesha kazi za kutokana na mchakato mrefu wa kufuta upimaji huo wa zamani ndani ya kipindi cha mkataba wa kazi kabla ya kuanza upimaji mpya.

Pia suala la matumizi mbaya ya fedha za michango ya wananchi kwa ajili ya urasimishaji kutokana na usimamizi hafifu wa Mamlaka za Upangaji kwa Kamati za Urasimishaji makazi lilichangia kwa kiasi kikubwa kuchelewesha zoezi hili. Maeneo ambayo yalikumbwa na changamoto hii ilikuwa ni lazima suluhu ipatikane aidha kwa mazungumzo au kisheria ndipo urasimishaji uendelee.

Aidha Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Ruvuma akatumia nafasi hii kumuomba Mkuu wa Mkoa kuhimiza watumishi wa mkoani hasa idara za ardhi kuhakikisha wanawajibika kwa wakati kutekeleza kazi zote zinazowajia ili kupunguza malalamiko ya ucheleweshwaji wa hati.





# UTATUZI WA MIGOGORO YA ARDHI

**Na Lusajo Mwakabuku**







Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Ruvuma Ndg Ildefonce Ndemela kwa kushirikiana na Wataalam kutoka Ofisi ya Ardhi Mkoa pamoja na Ofisi ya Ardhi Tunduru wakisikiliza na kutatua kero na malalamiko mbalimbali ya wananchi katika Halmashauri (W) Tunduru. Hii ni hatua ya utekelezaji wa Agizo la Mh. Lukuvi la kuhakikisha Ofisi za Mikoa zinatembelea wananchi na kuwasikiliza kero zao.

Aidha kwa mwaka wa fedha 2020/21 Mkoa wa Ruvuma umepangiwa kutatua migogoro 105. Hadi sasa Mkoa umetatua Migogoro 89 kati ya migogoro 98 iliyowasilishwa kutoka katika Halmashauri 8 zilizopo Mkoa wa Ruvuma. Migogoro 9 iliyobakia bado inaendelea kuratibiwa na kutafuta njia bora za kumaliza kabisa malalamiko hayo.

Katika kuhakikisha Migogoro na kero mbalimbli za wananchi zinatatuliwa kwa wakati, Ofisi ya Ardhi Mkoa imepanga kila siku ya Jumatano ya kila week inatembelea Halmashauri moja kati ya Halmashauri 8 zilizopo ili kwenda kusikiliza na kutatua kero hizo.

Akielezea aina za migogoro inayotawala mkoani Ruvuma, Ndemela alisema Migogoro kati ya mwananchi na mwananchi ndio mingi ingawa haitajwi sana kwakuwa haina sauti kubwa sana. Migogoro hii kusababishwa na wananchi kutoheshimu taratibu za umiliki ardhi hasa iliyopimwa na kumilikishwa. Pia wapo Wananchi wanaouza ardhi za familia bila kuwa na Kibali cha familia. Pindi mwanachi aliyenunua anapotaka kuendeleza hukumbana na pingamizi kutoka kwa wanafamilia wanaodai kutotambua mauziano.

Wakati mwingine wataalam wanaingia katika kadhia hii hasa wakati wa umilikishaji kwa kuwa mtalaam anaweza kuendelea na taratibu za Umilikishwaji kwa kutumia nyaraka za mauziano yasiyo na Kibali cha familia. Pindi malalamiko yakijitokeza Serikali inakuwa sehemu ya Mgogoro huo.

Kamishna wa Ardhi Msaidizi wa Mkoa wa Ruvuma ameziagiza ofisi zote za Ardhi zilizopo Halmashauri kuhakikisha zinapanga ratiba za kwenda kusikiliza kero kwa wanchi.





*Kamishana wa Ardhi Mkoa wa Ruvuma Ildefonce Ndemela akiwasilisha taarifa ya sekta ya Ardhi Mkoa wa Ruvuma*

# MALENGO MAPYA YA UTEKELEZAJI WA UHUISHAJI KUMBUKUMBU ZA MILKI ZA ARDHI

**Na Lusajo Mwakabuku**
WANMM

Katibu Mkuu alitoa maelekezo kwa mikoa yote nchini kuhusu kuhuisha kumbukumbu za Ardhi ili kufikia malengo la kukusanya mapato lengo ambalo wizara imepangiwa. Moja ya maelekezo hayo ilikuwa kila afisa katika sekta ya Ardhi kwenye kila Halmashauri apewe kitalu/vitalu vya viwanja na kusimamia kwa ufanisi ukusanyaji wa mapato. Orodha ya ugawaji wa vitalu kwa kila Afisa iliwasilishwa kwa Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Pamoja na kwamba maelekezo hayo ylifanyika lakini bado utekelezaji wa kazi hiyo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 hakufanyika kwa ufanisi mkubwa, baada ya kuliona hilo, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ameagiza zoezi hilo lianze upya kuanzia tarehe 01/07/2021 na kutoa taarifa kila Alhamisi ya kila wiki ya muenendo wa zoezi hilo kulingana na mgawanyo wa vitalu kwa wataalam. Kutokana na maelekezo hayo, mkoa umejipanga kuhakikisha kila Afisa katika kitalu/vitalu atakavyopewa atahakikisha anafanya kazi muhimu zikiwemo kutambua taarifa za kila kiwanja katika kitalu/vitalu kulingana na ramani zilizoidhinishwa na kisha kupata taarifa za wamiliki kulingana na taarifa za uwandani, anwani ya mmiliki, namba ya simu, na namba ya kitambulisho cha NIDA, kwa kulinganisha na taarifa zilizopo Ofisi za Ardhi.

Kamishna Msaidizi Mkoa wa Ruvuma pia ameagiza kila afisa ahuishe taarifa alizofanyia kazi za kila kiwanja katika mifumo ya utunzaji wa kumbukumbu za Ardhi na kupeleka Ankara za madai ya kodi kwa wamiliki wanaodaiwa kwa viwanja ambavyo upimaji wake umekamilika na siku tisini (90) zimepita, mmiliki atakiwa kupewa ankara ya umilikishaji ya siku thelathini (30) na asipolipa apewe ankara ya ulipaji kodi ya kiwanja husika. Kwa viwanja ambavyo upimaji wake utakamilika ndani ya mwaka wa fedha 2021/2022, mmiliki atapewa ankara ya umilikishaji na asipo lipa ndani ya siku tisini (90) atatakiwa kupewa ankara ya kulipia kodi ya kiwanja hicho.

Pia mkoa kumedhamiria Kusambaza Hati za madai ya kodi kwa wakati kwa wadaiwa sugu wa kodi ya Pango la Ardhi kwa kuanzia na wadaiwa wakubwa na pia Kufungua mashauri ya kodi kwa wakati katika Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kwa kaunza kwa wadaiwa wakubwa.



